# KIFO
## JUU YA
# MSALABA

# ?

**HOJA KUMI KUTOKA KATIKA BIBLIA TAKATIFU**

# KIFO JUU YA MSALABA
# HOJA KUMI KUTOKA KATIKA BIBLIA TAKATIFU.

**Kifo juu ya Msalaba**
**Hoja Kumi kutoka katika Biblia Takatifu**

**Mwandishi**
**Maulana Abul-Ata Jalandhari, H.A.**

**Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2011**
**Nakala 1000**
**Chapa ya pili Nakala 3000**
**Novemba, 2011**
**Chapa ya tatu Nakala 3000 – 2015**

**Kwa mawasiliano zaidi:**
**S.L.P  376 Dar es Salaam, Tanzania.**
**www.alislam.org.**

## SHUKURANI

Tunayo heshima na furaha kuweka kijitabu hiki mbele ya wasomaji watukufu wa lugha ya Kiswahili. Kijitabu hiki kiliandikwa na mtaalamu wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya, Maulana Abul-Ata Jalandhari, na kusambazwa katika lugha ya Kiingereza na Bwana Muhamad Saeed Ahmad Lone wa London.

Kutoka na faida ya kujitabu hiki, Bwana Muhammad Saeed Ahmad Lone alimuomba Bi Radhia Kaluta Amri Abedi, Rais wa zamani wa Lajna Imaillah Tanzania, akitafsiri katika Kiswahili, kazi ambayo ameifanya kwa ufundi. Bwana Mahmood Hamsin Mubiru ambaye ni katibu wa Malezi Tanzania na Mhariri wa gazeti la Jumuiya

la kila mwezi – “Mapenzi ya Mungu” – aliombwa ili akipitie.
Bi Twahira Swaleh Mbaruku Kapilima, Katibu Mkuu wa Lajna Imaillah1 Tanzania, naye pia akakipitia.

Halikadhalika Sheikh Jamil Rahmaan Rafiq aliyewai kuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Tanzania na Kenya pia likipitia.

Tunawashukuru wote ambao kwa njia moja au nyingine wamesaidia katika kufanikisha uchapaji wa kijitabu hiki muhimu.

---

[1]Lajnalmaillah-Idara yakinamamawaKi-Ahmadiyya.

Na neno letu la mwisho ni kuwa sifa zote

njema ni za Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu.

Msambazaji
Novemba, 2011

# UTANGULIZI

Marehemu baba yangu Maulana Abul-Ata Jalandhari, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu alikuwa msomi mashuhuri wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Alipata heshima na sifa maalum ya kuitumikia Jumuiya maisha yake yote. Alipata pia fursa ya kufanya kazi karibu sana na Khalifa mtufuku wa pili na wa tatu.

Kwa kutambua utumishi wake uliotukuka, Khalifa Mtukufu wa pili (Mwenyezi Mungu Awe radhi naye) alimpa lakabu ya Khalid (sahaba maarufu wa Mtukufu Mtume Muhammad, rehema na amani zimfikie) ambaye anasifika kwa ushujaa na mafanikio aliyokuwa akipata mwanzoni mwa historia ya Islam.

Pengine makala ndogo inaweza kusababisha athari kubwa kuliko ile ya kitbau kikubwa. Ni matumaini yangu kwamba hiki kijitabu kilichomo mikononi mwako kina athari kama hiyo.

Nakumbuka waziwazi mazingira ambamo baba yangu aliandika kijitabu hiki. Alikuwa mgonjwa wakati huo na alijitenga kwenye kijiji kidogo kijulikanacho kama Rambari huko Kashmiri-India ili apate nguvu. Kwa sababu ya ugonjwa wake mimi niliandika imla ya makala yote. Makala ilichapishwa kwanza katika toleo la kila mwezi la Al-Furgan – lililohaririwa na baba yangu. Baadaye tafsiri ya Kiingreza ilitokea katika "Muslim Herald" linalochapishwa na "London Mosque". Baadaye makala hiyo ilichapishwa kama kijitabu na kusambazwa sana.

Natumaini kwamba msomaji ataithamini makala hii fupi na fasaha. Simulizi yake ni yenye nguvu ya hoja na yenye kuaminisha. Hoja kumi kutoka katika Biblia Takatifu zimetolewa ndani yake. Hizi zinathibitisha kwa ushahidi dhana potofu juu ya imani ya sasa ya Kikristo kuhusu kifo cha Yesu Kristo (amani ya Mungu iwe juu yake) msalabani.

Hoja hizi zimetolewa kutoka katika Biblia na kuelezwa wazi ili kusibakie utata. Kilipochapishwa mara ya kwanza kijitabu hiki, kilithibitika kupendwa na kuwa chenye manufaa. Ningependa kunukuu mfano mmoja wa athari yake katika maisha ya bibi mmoja Mkristo, Bibi Selma Saeed Khan, alinisimulia kwamba wakati hayati Saeed Khan aliyekuwa akimhubiri ambaye hatimaye alimpa kijitabu hiki asome,

kilitikisa kiini cha msingi wa imani yake. Alisema baada ya kukisoma, alitambua kwamba hoja zilizotolewa lazima zitiliwe maanani. Kwa maneno yake mwenyewe. "Kijitabu hiki kimethibitika kuwa cha muhimu sana kwa safari yangu ya kiroho kuelekea Islam."

Baada ya kukichunguza kitabu hiki, anasimulia, kwamba aliifikiria imani ya uhai na kifo cha Yesu kwa makini sana na mara aliridhika kwa hisani ya Mwenyezi Mungu hatimaye akaamua kusilimu. Ninafurahi kuongeza ya kwamba Bibi Selma Khan amejitolea kuwa mhubiri mwenye bidii wa Islam kwa kadiri ya uwezo wake. Kwa juhudi zake watu wengi wa Uiongereza wameongezwa kwenye njia ya Islam. Mwenyezi Mungu ambariki kwa kumpa

umri mrefu na mafanikio zaidi kwa kazi nzuri. Ninatoa shukrani maalum kwa ndugu yangu Muhammad Saeed Ahmad Lone wa London ya Mashariki ambaye amejitolea kuchapisha kijitabu hiki kwa gharama yake kwa idhini ya Jumuiya ya Waislam Ahamadiyya. Mwenyezi Mungu Amlipe na kubariki uenezaji wa chapa hii. Amin

Ataul Mujeeb Rashid
Imamu wa London Mosque
7 Augusut, 2010

# JINSI NILIVYOKUWA MWISLAM - AHMADIYYA

Miaka arobaini iliyopita nilisoma kijitabu hiki. Ilinichukua dakika chache tu kukisoma lakini kilisaidia kubadilisha maisha yangu daima.

Mimi ni bibi wa Kiingereza na nililelewa kama muumini wa madhehebu ya Methodisti huko Yorkshire England. Babu yangu alikuwa mhubiri nami nilikuwa mwalimu wa Sunday School. Niliposoma "Kifo juu ya Msalaba" mnamo mwaka 1963, nilikuwa mwanafunzi wa uuguzi niliyesajiliwa na Serikali nikitayarishwa kwenda bonde la Zambezi huko Afrika kama Mmisionari wa Kikristo.

Nilikuwa na Imani isiyopingika ya Ukristo, lakini nikaja tambua kuwa licha ya elimu nzuri ya Biblia nilijua kidogo kuhusu imani nyingine. Nilidhani inafaa kupata uelewa zaidi wa dini nyingine endapo nataka kuwabadili wengine kwa urahisi kuwa Wakristo, hivyo nilisoma vitabu kuhusu mlinganisho wa dini nikijaribu kupata uelewa wa imani mbalimbali zikijumuisha Uhindu, Ubudha na Islam.

Nilikuwa pia mwanachama wa kikundi cha majadiliano ya kidini katika hospitali yangu lakini wanachama wake wote walikuwa Wakristo, kama walivyokuwa wazungumzaji walioalikwa. Kufuatia

masomo yangu ya baadhi ya vipengele vya Islam niliuliza maswali ambayo nilihitaji majibu ili niiridhishe dhamiri ya imani yangu. Sikuridhishwa na mara kwa mara niliambiwa na Makasisi, Mapadri na Wachungaji mbalimbali waliowakilisha makanisa tofauti "uwe tu na itikadi na imani."

Kutoridhika kwangu kulikoongeka kulinifanya nisome idadi kubwa ya vitabu vya dini na niliomba mwongozo. Nilikumbuka maelekezo ya Kristo: "Ombeni na mtapewa,tafuteni na matapata pigeni hodi mtafunguliwa." Nilisoma nikaomba a kujadili imani na marafiki na wafanyakazi wenzangu katika jitihada zangu za kutafiri.

Nilitumia miezi mingi katika hali hii ya kutotulia wakati kijana mmoja daktari aliyekuwa wodini kwangu alinipa hiki kijitabu unachokishika sasa.

Nilikisoma, na kwangu kilionekana kuwa ni jibu la Mwenyezi Mungu kwa maombi yangu. Ilikuwa kana kwamba mwanga umewashwa, maswali yangu hatimaye yanajibiwa, nikarudishiwa amani. Kwa Fadhili ya Mwenyezi Mungu nikawa Mwislam wa Ahmadiyya, mara baadaye, wakati wa Hadhrat Mirza Bashirudin Mahmood Ahmad. Khalifatul-Masihi II r.a. (kiongozi wa Ahmadiyya wakati huo).

Ninapendekeza kwa yeyote atafutaye

ukweli kuwa asome kijitabu hiki na amwombe Mwenyezi Mungu msaada wake na mwongozo katika safari ya kuelekea Kwake.

Selma Mubaraka Saeed Khan
Fridene, Yorkshire, England
Februari, 2004

## KUZALIWA (UZAO) KWA YESU

La ajabu ni kwamba wafuasi wa dini kuu tatu duniani yaani Wayahudi, Wakristo na Waislamu wanatofautiana kuhusu kuzaliwa na kifo cha Yesu Kristo, aliyezaliwa miongoni mwa Mayahudi.

Wanaitakidi kuwa kuzaliwa kwake kulikuwa ni kwa haramu na wanatoa masingizio dhidi ya Mariamu, mama yake Yesu. Wanamtangaza kuwa mwana haramu (Mungu apishe mbali) na hivyo kutostahili *"kuwa katika mkusanyiko wa watu bwana"*. Wakristo kwa upande mwingine wanaamini ya kuwa Yesu Kristo alizaliwa bila baba

na hivyo akawa ni mwana wa Mungu. Hii inaonesha Wayahudi na Wakristo wana mitazamo tofauti iliyopita kiasi kuhusu kuzaliwa kwa Yesu. Waislamu kwa upande wao hawana shaka juu ya Yesu kuzaliwa bila baba, lakini sio mwana wa Mungu. Kuzaliwa bila baba linaweza kuwa tukio la ajabu kidogo lakini sio kinyume na maumbile. Ipo mifano katika historia ya utabibu inayoonesha kuwa mabikira walipata watoto. Hata Adamu anayekubalika kuwa mwanzilishi wa kizazi hiki cha sasa alizaliwa bila ya kuwa na baba wala mama. Hii ni imani ya dini zote tatu tulizokwisha zitaja. Waislamu wanaamini kuzaliwa kwake bila ababa hakuna uhusiano wowote na kuwa mwana wa Mungu au utakatifu. Alikuwa ni binadamu na sio zaidi ya hivyo. Yesu mwenyewe alijiita mwana wa Adamu katika Agano jipya.

## KIFO CHA YESU

Kifo cha Yesu halikadhalika ni swala lenye utata miongoni mwa Wayahudi, Wakristo na waislamu. Wayahudi wanaamini kwamba Yesu alifia msalabani kwa sababu alikuwa Nabii Muongo. Jambo hili wanalitolea ushahidi kutoa kwenye Biblia, "na ikiwa mtu ametenda dhambi inayostahili kifo, na akifa na ukimuamba msalabani huyo amelaani na Mungu. (Mwanzo 21:22-23).
Sawa na imani yao Yesu alikuwa Nabii muongo, hivyo alifia msalabani ikiwa ni alama ya mtu aliyelaaniwa na Mungu.

Wakristo wao wanaamini ya kuwa Yesu aliwambwa msalabani na akafa kifo cha laana. Paulo anasema:

"*Kristo alitukomboa katika laana ya Torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu*

*maana imeandikwa amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti" (3:13).*

Lakini Kurani Tukufu inatanagz akuwa Kristo hakufa msalabani. Mwenyezi Mungu alimuepusha na kifo cha kusulubiwa kama alivyo wanusuru wapendwa wake kutokana kwenye mateso. Je Yona hakutoka mzima kutoka kwenye tumbo la nyangumi? Ukweli ni kwamba Yesu Kristo alizimia pale msalabani, lakini alipoondolewa pale msalabani alirejewa na fahamu na baadaye akafa kifo cha kawaida akiwa na umri wa miaka 120

Kwa ushahidi mzito wa imani yao kuwa Yesu Kristo alikuwa nabii muongo Wayahudi hususana mafarisayo wa wakati wake walitunga masingizio mazito wa kisiasa ya kwamba hakua mtiifu kwa Mfalme wa Rumi na kwamba alikuwa amedai kuwa Mfalme

wa Wayahudi. Gavana Pilato hakuamini kuwa Yesu alikuwa na hatia lakini kwa sababu ya hofu ya umati wa Wayahudi, alimtoa Yesu aende kusulubiwa.

Walimuweka msalabani, ambapo alikaa kwa saa tatu au nne tu na halafu akaondolewa akiwa katika hali ya kuzirai na kuwekwa kwenye pango lililokuwa kwenye shamba karibu na tukio.

Kifo kwa njia ya kusulubiwa kilikuwa kinachukua siku nyingi. Mtu aliyewekwa msalabani alikumbana na madhila ya njaa na kiu na aghalabu miguu yao ilivunjwa. Walikufa kifo kilichochukua siku nyingi. Lakini haikuwa hivyo kwa Yesu Kristo. Kama ilivyotokea, yeye aliwekwa msalabani Ijumaa alasiri na siku iliyofuata ikiwa ni Sabato siku ya wayahudi – hakuna mwenye hatia aliyeruhusiwa kuwa kwenye msalaba katika siku hiyo takatifu, hivyo aliondolewa pale msalabani baada ya saa tatu au nne.

Kupoteza damu kwa wingi kulimfanya zirai. Alidhaniwa ya kuwa amefariki. Mwili wake uliwekwa kwenye pango lililokuwa kwenye bustani ya Yusufu wa Arimathaya ambaye alikuwa mwanafunzi wake. Yesu akiwa bado mzima katika pango lile alitoka katika pango (kaburi) lile siku ya tatu ilhali amejificha

Akakutana na wanafunzi wake mahali panapoitwa Galileya na akala nao chakula. Vidonda vyake viliponeshwa na dawa ya kuchua ambayo ilikuwa imetayarishwa mahsusi na wanafunzi wake.

Hii ndiyo hadithi ya kusulubiwa kwa Yesu. Maelezo ya wak juu wa kifo chake sio tu kwamba ni kinyume na maumbile bali ni kinyume pia na ushahidi wa historia na mantiki. Wanaamini ya kuwa Yesu hasa alifia msalabani na siku ya tatu alipaa kwenda mbinguni. Lakini ikithibitishwa kwamba

hakufa msalabani na wala hakufufuka kutoka wafu basi msingi mzima wa imani ya Kikristo unavunjika. Paulo ambaye ndiye hasa mwanzilishi wa ukristo kama tunavyo ufahamu hivi leo anasema:

*"Tena kama Kristo hakufufuka, basi kuhubiri kwetu ni bure na imani yetu ni bure. (Wakorintho 15:14).*
*Hayati Dr. Zwemar mmishionari maarufu wa Kimarekani anasema:*
*"Kama imani yetu juu ya kifo cha Kristo si sahihi basi ukristo mzima ni uongo mtupu"*

## 1. ISHARA YA YONA.

Sasa tunaendelea na hoja zetu kutoka kwenye Biblia za kuonesha kuwa Yesu hakufia msalabani. Tunasoma katika Agano Jipya.

*Na makutano walipokuwa wakimkusanyikia, alianza kusema, kizazi hiki ni kizazi kibaya, kinatafuta ishara, wala hakitapewa ishara kwa waniwawi, ndivyo atakavyokuwa mwana wa Adamu kwa kizazi hiki. (Luka 11:29-30).*

*Tena akasema, Akajibu, akawaambia kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya Nabii Yona. Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu, mchana na usiku katika tumbo la nyangumi hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.*

*(Jonah 1,17, 2:1,2).*

Hapo Yesu Kristo analinganisha kadhia yake na ile ya Nabii Yona. Je Yona aliwapa ishara gani watu wa Ninawi. Biblia inasema:

*(Jonah 1,17, 2:1,2).*

*Bwana akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa siku tatu, mchana na usiku. Ndipo Yona akamwomba Bwana, Mungu wake, katika tumbo la yule samaki akasema: Namlilia Bwana kwa sababu ya shida yangu naye akaniitikia, katika tumbo la kuzimu naliomba, nawe ukasikia sauti yangu.*

Sawa na aya hizi za Biblia, Jona alimezwa na samaki mkubwa na kawa katika tumbo la samaki huyu siku tatu na mausiku matatu na hatimaye akatoka katika tumbo hilo la samaki ilhali ni mzima. Hiyo ni ishara waliyopewa watu wa Ninevatani, Jona aliomba akaokolewa wakati yumo katika tumbo la samaki. Mungu alisikia maombi yake na Yona akatoka katika tumbo hilo akiwa ni mzima. Yesu anasema kizazi

hiki kiovu na cha zinaa hakitapewa ishara isipokuwa kama ile ya Yona. Kwa hiyo ni nini kilicholeta kufanana baina ya ishara ya Yona na Yesu. Hakuna isipokuwa ukweli ya kwamba kuingia katika tumbo la samamki na kuingia katika moyo wa ardhina kutoka humo wazima. Yona na Yesu walilia kutokana na hayo yaliyowasibu na wakamuomba Mola awaokoe. Maombi ya wote wawili yalipokelewa. Kama Yesu hakuingia katika moyo wa nchi akiwa ni mzima na kutoka humo akiwa ni mzima, kuko wapi basi kufanana baina ya ishara hizi mbili? Yesu aliahidi kuonesha ishara moja tu kwa kaumu ya wakati wake, lakini hata kama ishara hiyo itathibitishwa kuwa si kweli, je kuna jingine la kuthibitisha madai yake ya kuwa Mtume? Kurejea kwa Yesu kwa ishara ya Yona ina maana ya kuwa hatakufa mslabani. Kwa hiyo kuna kila sababu ya kuamini kuwa nadharia ya kuzirai haikujengwa kwenye nadharia tete.

## 2. MKE WA PILATO AONA NJOZI

*Na alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpeleka mjumbe kumwambia usiwe na neno na yule mwenye haki, kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake (Mathayo 27:19).*

Njozi ya mama yule ilikuwa ya kweli na iliyokuja wakati muafaka. Iliashiria kunusurika kwa Kristo kutokana na kifo cha laana kwenye msalaba. Mwenyezi Mungu huwaokoa waja wake kwa kupitia njozi za watu wengine kama ilivyotokea kwa Yusuf alipotoa taawili juu ya njozi mbili alizoziona Farao na akaachiliwa kutoka gerezani. Mwenyezi Mungu alitaka kumlinda Yesu dhidi ya maadui zake na ndio maana ya njozi ya mke wa Gavana wa Kirumi. Na njozi hii ilimuathiri Gavana huyu alipokuwa anatoa hukumu yake.

## 3. MWELEKEO WA HURUMA WA GAVANA WA KIRUMI

Wayahudi waliipeleka kesi ya Yesu Kristo kwa Pilato, Gavana wa Kirumi wa Falestinia. Alifanya utafiti wa kisheria na hatimae akatangaza kuwa hakuwa na makosa yaliyokuwa katika mashataka. Aliwaambia. *"Mtu huyu mmemleta kwangu kana kwamba anapotosha watu, nami tazama nimeamua mambo yake mbele yenu, ila sikuona kwake kosa lolote katika mambo hayo mliyomshitaki". Luka 23:14.*

*Akawatokea way tena, akawaambia mimi sioni hatia yoyote kwake. Lakini kwenu kuna desturi ya mimi kuwafungulia mtu mmoja wakati wa Pasaka, basi mwapenda, niwafungulie mfalme wa Wayahudi? Basi wakapiga kelele tena kusema, si huyu, bali Baraba, naye yule Baraba alikuwa*

*mnyang'anyi. (18:38,40).*

*Na tangu hapo Pilato akatafuta kumfungua lakini Wayahudi wakapiga makelel wakisema, ukimfungulia huyu, wewe si rafiki yake Kaisari, kila mtu ajifanyaye kuwa mfalme humfitini Kaisari.*

Kutokana na nukuu zilizotolewa hapo juu, ni dhahiri ya kwamba Gavana alimuona Yesu asiye na hatia sawa na mashataka ya Wayahudi dhidi yake, alijitahidi kwa uwezo wake kumuachilia lakini Wayahudi walipotia kani kumtaarifu Kaisari huko Roma, alisalimu amri kwao na kumkabidhi Yesu kwao lakini kwa njia ya siri alifanya mikakati ya kumuokoa Yesu. Njozi ya mkewe ilikuwa mbele yake na alimaizi kuwa makuhani walikuwa wamekula njama dhidi yake kwa sababu ya wivu na husuda.

## 4. MIKAKATI YA PILATO KUMUOKOA KRISTO.

Pilato, Gavana alikuwa na imani thabiti kuwa Yesu Kristo hakuwa na hatia, hivyo tangu awali alitengeneza mikakati ya kumuokoa. Kama afisa anayewajibika kwa himaya ya Roma asingeweza kuonesha dhahiri mikakati yake ya kumsaidia Yesu Kristo, lakini yeye ndiye alikuwa uti wa mgongo wa mipango hiyo. Wahusika wengine katika mikakati hiyo ni pamoja na Yusufu wa Arimathea, diwani mwenye heshima na mfuasi wa Yesu Kristo. Mhusika mwingine katika mikakati hiyo alikuwa msomi mmoja Nikodemasi ambaye alifahamu fika mikakti yote. Tunasoma katika Yohana: *Akaenda Nikodemas naye, yule aliyemwendea usiku hapo kwanza akaleta mchanganyiko wa manemane na udi yapata ratili mia).*

Pilato alifanya jambo la busara sana la kuchagua Ijumaa alasiri kuwa siku ya kumweka Yesu msalabani ili asiendelee kuwa msalabani jua likichwa, siku iliyokuwa inafuata ilikuwa Sabato, siku takatifu ya Wayahudi. Aliwachagua Yusufu na Nikodemasi marafiki wa karibu wa Yesu Kristo kukamilisha makakati huu uliokuwa tayari umekwisha pangwa. Hatua zote za kumfanya Yesu apate fahamu tena zilichukuliwa. Kama si hivyo Nikodemas alikuwa na maana gani kuleta mchanganyiko wa manemane na udi. Katika kumbukumbu za Serikali Yesu alielezwa kuwa amekufa ili kuwatuliza Wayahudi na Serikali ya huko Roma. Kwa ushujaa mkubwa Yusufu wa Arimathaya aliomba mwili wa Yesu kutoka kwa Gavana na bila kusita akapewa. Kama mkakati huu haukuwa umepangwa, Gavana angempaje mwili wa Yesu mtu ambaye si mweneyeji asiyejulikana? Kuna sababu

ya kuamini kuwa hata Yesu Kristo naye aliufahamu mkakati huu ili bishara ile itimie kwani kama Yona alivyokuwa katika tumbo la samaki siku tatu mchana na usiku hivyo hivyo mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku. Kukutana kwa Nikodemasi na Yesu Kristo usiku uliopita kunaweza kueleza kutokana na nadharia hii.

## 5. MUDA WA KUSULUBIWA

Muda wa kuwa msalabani kwa Yesu haukutosha kumfanya Yesu afie pale msalabani. Wahalifu kwa desturi walichukua siku nyingi kufa kifo cha kukawia kwa sababu ya kupoteza damu kutoka kwenye vidonda vya mikononi na miguuni, kuchoka kwa mwili na maumivu, nja na kiu. Kwa akali saa za kufa msalabani zilikuwa kati ya saa

24 na 24, lakini matukio mengine ilichukua siku nyingi kufia msalabani. Hali ya namna ilipojitokeza ilikuwa lazima kuvunja miguu ya wahalifu ili kifo kitokee kwa sababu ya kupoteza damu.

Hebu sasa tuchunguze kusulubiwakwa Yesu. Agano Jipya linatumabia kwamba Yesu alikuwa msalabani kwa saa chache tu. Muda hasa aliokaa Yesu msalabani haukuzidi saa tatu au nne. Yesu Kristo ambaye alikuwa bado katika utonvu wa ujana (miaka 33) na mwenye afya nzuri hakutarajiwa kuwa amekufa kwa muda mfupi hivyo ukikumbuka kuwa miguu yake haikuvunjwa kama ilivyofanywa kwa wezi wawili waliosulubiwa pamoja naye.

Haitakuwa nje ya mada tukisema kuwa sawa na Kalenda ya Kirumi siku ilianza kuchomoza kwa jua na kuisha kwa kuzama

kwa jua. Mwenendo huu bado unafuatwa hata hivi leo huko nchi za Uarabuni. Sawa na Yohana (19:14) ilikuwa ni saa sita ya siku ya Ijumaa wakati Pilato alipozungumza na Wayahudi kuhusu kusulubiwa kwa Yesu na kumkabidhi Yesu kwao.

*"Na ilipokuwa saa sita, palikuwa na giza juu ya nchi yote, hata saa tisa. Na saa tisa Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu Eloi, Eloi lama Sabakthani? Maana yake, Mungu wangu mbona umeniwacha?*

Hii inaonekana Yesu alikuwa na fahamu zake mpaka saa tisa alasiri, halafu akapoteza fahamu. Hii ndiyo waandishi wa Agano Jipya wanayoita.......... Hakuna mwandishi wa Agano Jipya aliyekuwepo kwenye eneo la tukio ili kutoa ushahidi wa kuona. Kuzirai kulichukuliwa kuwa ni kifo msalabani

maana yake ni laana. Je hatusomi katika Biblia kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu. Ni ushupavu wa kiasi gani kudiriki kwa Wakristo kumuita Nabii mkweli wa Mungu kuwa amelaaniwa na Mungu?

## 6. KUTOKA KWA DAMU NA MAJI

*Basi askari wakaenda wakamvunja miguu wa kwanza, na wa pili aliyesulubiwa pamoja naye. Lakini walipomjia Yesu na kuona ya kuwa amekwishakufa, hawakumvunja miguu, lakini askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki na mara ikatoka damu na maji (Yohana 19:32, 33, 34).*

Askari hawakuvunja miguu ya Yesu kwani walichukulia kwamba tayari amekwishakufa kumbe kwa yakini alikuwa amezirai tu au

kuwanyamazisha Wayahudi wenye hasira ilitangazwa kuwa tayari amekwisha fariki. Lakini kwa njia moja ama nyingine askari alimchoma ubavu kwa mkuki mara ikatoka damu na maji ambayo ni alama ya uhai kwani damu na maji havitoki katika mwili wa maiti. Kuna jambo la kutafakari hapo kwa wale ambao wanajali kufikiri.

## 7. HAKUNA ALIYESHUHUDIA TENDO LA KUSULUBIWA.

Waandishi watatu wa Injili wanaeleza ya kuwa palikuwpo na giza nchi nzima kutoka saa sita hadi saa tisa na palikuwepo na tetemeko na miamba ilipasuka na mapazia hekaluni yalipasuka. Uzoefu wa kila siku unaeleza ya kuwa siku ya upepo namna hii unaombatana na tetemeko watu hukimbilia makwao na hawakai kuangalia

jambo lolote jingine linalotisha. Hebu fikiri kidogo nani angeweza kusimama na kutoa ushahidi wa kuona ili kueleza kuwa Yesu hasa alikufa msalabani. Wayahudi, kama walikuwa mahali pale penye tukio, bila shaka walikimbia tufani hiyo na kutetemeka kwa ardhi na wote kukimbilia majumbani mwao. Na wanafunzi wa Yesu tayari walikuwa wamekwisha kimbia kutoka mahali alipowekwa msalabani.

*"Akaanza kulaani na kuapiza, simjui mtu huyu mnayemnena. (Marko 14:71)*.

*Ndipo wakamwacha, wakakimbia wote. (Marko 14:50).*

Kufupisha, hakuwepo mtu kwenye tukio hilo ambaye angesema kwa uhakika kabisa kwamba alimuona Yesu akikata roho. Hayo yote ni kudhani na kufikirika.

# 8. UJUMBE WA YESU KWA KONDOO WALIOPOTEA WA ISRAELI

*Kwa mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea – (Luka 19:10).*

*Na kondoo wengine ninao ambao si wa zizi hili, na hao nao imenipasa kuwaleta na sauti yangu wataisikia, kisha kutakuwepo kundi moja na mchungaji mmoja. (Yohana 10:16).*

*Akawaambia imenipasa kuihubiri habari njema ya Ufalme wa M katika miji mengine pia, maana kwa sababu hiyo nalitumwa. (Luka 4:43).*

*Akajibu akasema, sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba wa Israeli (Mathayo 15:24).*

Ni dhahiri kutoka kwenye nukuu hizo hapo juu kwamba ujumbe wa Yesu ulitabiriwa uwafikie makabila yote kumi na mbili ya Israeli yaliyokuwa yamesambaa nchi za Mashariki kuanzia Falestina hadi India katika kipindi alichodhihiri Yesu. Kati ya makabila kumi na mbili ya Israeli wakati ule ni makabila mawili tu yaliyokuwa Falestina wakati yale kumi yalikuwa yamesambaa kutoka Falestina hadi India. Haiwezekani kusemwa kuwa Yesu alikamilisha kazi yake kama hakuyahubiri mataifa yote mengine kumi ya wanakondoo wa Israeli waliopotea. Kifo kinachofikiriwa cha Yesu msalabani akiwa na umri wa miaka 33 ni pigo kwa kazi aliyotumwa aifanye. Ukweli ni kwamba, Yesu Kristo alipokwisha okoka na adha ile ya msalabani, alihamia mashariki kuwatafuta kondoo waliopotea na jambo hili linao ushahidi tosha wa

kihistoria, ushahidi ambao unaungwa mkono na uvumbuzi wa elimukale. Yesu aliwapata kondoo waliopotea huko Persia, Afghanistan na Kashmir na kuwahubiri hadi akapata mafanikio makubwa kuliko yale aliyoyapata Falestina. Alikufa kifo cha kawaida na kuzikwa Srinaga Kashmir.

## 9.USHINDI WA YESU DHIDI YA MAADUI ZAKE.

*Akizungumza na wanafunzi wake Yesu anasema: Tazana saa yaja, na imekwisha kuja, ambayo mtatawanyika kila mmoja kwao kwao na kuniacha mimi peke yangu, walakini mimi si peke yangu, kwa kuwa baba yupo pamoja nami. Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu, ulimwenguni mnayo dhiki lakini jipeni moyo, mimi nimeushinda ulimwengu (16:32-33).*

Sasa, ushundi huo wa Yesu unatokanana na nini? Kifo chake msalabani au kuepukana na kifo hicho? Kama alikufa msalabani basi ni Wayahudi walioshinda kwani dhamira yao ilikuwa ni kudhihirisha kuwa alikuwa muongo kwa kujiita Masiha. Na katika hili walikuwa na msaada wa kauli ya Biblia, kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu (Kumbukumbu la Torati 21:23). Lakini tukiamini kuwa alitolewa mslabani ilhali ni mzima (bila shaka akiwa katika hali ya kuzirai) na kwamba akatoka humo angali mzima hapo bila shaka ana haki ya kusema kuwa amewashinda maadui zake na kusambaratisha mikakati yao michafu. Yesu anaema:

*"Kama Yona alivyokuwa ishara kwa watu wa Ninevi hivyo hivyo mwana wa Adamu atakuwa ishara kwa kizazi hiki.*

Kwa maneno mengine Yesu aliwaambia Wayahudi kuwa Mola Mwenye Enzi angeweza kumuokoa kutoka kwenye makuchayakifokamavilevilealivyomuokoa Yona kutoka katika tumbo la samaki. Kushabihiana kwa mifano hii kunaweza kuwa kweli tu ikiwa Yesu anaingia katika moyo wa ardhi (kaburi) akiwa mzima na akatoka humo angali mzima.

## 10. MAOMBIYAKE YALIKUBALIWA

kusoma kwetu Biblia kunadhihirisha kuwa M huyasikiliza maombi ya Mitume wake na kuwaokoa na mateso na mitihani. Katika Agano Jipya tunasoma:

Tena tunasoma:

*Yesu akainua macho yake juu akasema, Baba nakushukuru kwa kuwa umenisikia nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia*

*siku zote, lakini kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya ili wapate kusadiki kwamba ndiwe uliyenituma. (Yohana 11:41-42)*.

Akasema, *Aba, Baba, yote yawezekana kwako, uniondole kikombe hiki, walakini si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe. (Marko 14:36)*.

Sawa na nukuu hizo hapo juu ni dhahiri Yesu aliogopa sana kuwekwa msalabani, hivyo aliomba kwa moyo mmoja aondolewe kikombe hicho kichungu. Yesu aliomba kwa unyenyekevu wa hali ya juu ili aondolewa aibu ya kufa kifo cha laana cha msalabani, angediriki vipi basi kwamba alikuwa ameishinda dunia kama angefia msalabani, kazi yake yote ingeharibika na wale wenye dhambi wangedadisi juu ya

ukweli wa madai yake ya kuwa Nabii. Fikra ya yeye kufa msalabani haikubaliki. Akiwa Nabii wa Mwenyezi Mungu hakuogopa kifo hiki chakawaida, alichoogopa ni kifo cha msalabani kwani kifo cha namana hii kingeweza kueleweka kuwa ni kifo cha laana jambo ambalo lingekuwa kinyume na ujumbe wake wa kitume.

*Siku hizi za mwili wake alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu (5:7).*

Hivyo inatubidi tuamini kwamba maombi hayo ya unyenyekevu wa hali ya juu bila shaka yalipokelewa na kimiujiza akaepukana na kifo cha msalabani na akaishi muda wa kutosha wa kuweza kufikisha ujumbe wake kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli huko mashariki:


Akawaambia, *imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika Miji mingine pia, maana kwa sababu hiyo nalitumwa.*

Ndugu wapendwa. Hoja hizi zinadhihirisha kwa fikra hizi za kusulubiwa kwa Kristo hazina ushahidi kutoka kwenye Biblia yenyewe. Hivyo ni wazi kuwa imani ya Kikristo iliyojengwa kwenye msingi huo mbovu haiwezi kuwa imara.

## ENYI WAPENZI


Hoja hizi zinathibitisha kuwa wazo la kifo cha Yesu kwa kusulubiwa halithibitiki hata kutokana na mtazamo wa Biblia. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba imani ya sasa ya Ki-kristo msingi wake hauko sahihi wala hauna maana.

**Kwa maelezo zaidi tizama katika tovuti: www.alislam.org**



**Picha ya Kaburi la Bwana Yesu Kristo (amani ya Mungu iwe juu yake) lililopo Mohallah Khanyar SRINAGAR, KASHMIR, INDIA jinsi linavyoonekana kwa nje.**

**Picha hii imepigwa na Bwana Mohammad Saeed Lone wa London.**



**Picha ya Kaburi la Bwana Yesu Kristo (amani ya Mungu iwe juu yake) lililopo Mohallah Khanyar SRINAGAR, KASHMIR, INDIA jinsi linavyoonekana kwa ndani.**

**Picha hii imepigwa na Bwana Mohamed Saeed Lone wa London.**